# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL8

# KISWAHILI PAPER 3 QUESTION

## SEHEMU YA A (Alama 20 )

**TAMTHILIA**

1. **Mstahiki Meya: Timothy Arege.**

**1. Lazima**
"Nilikusahau lini…? Mtu haukati mkono unaomlisha."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Taja na ueleze mbinu ya kifasihi iliyotumika kwenye dondoo. (alama 2)

c) Eleza sifa mbili za msemewa . (alama 4)

d) Kwa kutoa mifano mitano, thibitisha kuwa Wanacheneo waliukata mkono uliokuwa ukiwalisha. (alama 10)

## SEHEMU YA B: (Alama 20 )

**RIWAYA**

2. **Kidagaa Kimemwozea: Ken Walibora.**

**Jibu swali la 2 au la 3.**

2. … "alisimama jadidi na kuwatazama hawa watu wawili waliosimama wima kutetemeka kama waliopigwa na dhoruba ya theluji."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza hulka ya mrejelewa. (alama 6)

c) Jadili mchango wa wanawake katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 10)

3. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumiwa na mwandishi wa riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)
i) Majazi

ii) Kinaya

## SEHEMU YA C (Alama 20 )

**HADITHI FUPI**

3. **Damu Nyeusi na Hadithi nyingine – Ken Walibora na S.A Mohammed.**
**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** a) Eleza ufaafu wa anwani "Ndoa ya Samani" ya hadithi hiyo. (alama 2)

b) Eleza maudhui yoyote tisa katika hadithi ya "Ndoa ya Samani". (alama 18)

**5.** "Asanteni sana kuja. Sisi … hukabiliana na mengi."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Fafanua matukio yaliyosababisha mkutano huu. (alama 4)

c) Eleza changamoto sita , zinazoikumba jinsia ya kike katika hadithi husika. (alama 12)

## SEHEMU YA D (Alama 20 )

### USHAIRI

4. 6. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Sema semea wajibu, mwenye kutetema,
Sema na watu karibu, mbali ukisema,

Sema kufunza wajibu, noleji hekima,

Sema ajue fulani, usihulu sema.

Sema yanayokukaa, yanavyokusakama,

Sema yaliyozagaa, kwa ubwako mtima,

Sema unajihadaa, kwani twawafuma?

Sema wajue ni nani, usiache sema.

Sema yote si uasi, si tenge si noma,

Sema toa wasiwasi, upate salama,

Sema japo ni risasi, longa litauma,

Sema yote hadharani, radidia sema.

Sema pasi na ukali, mwiza taloloma,

Sema neno la asali, 'taramba'kitema,

Sema kwa mzo akili, watakushituma,

Sema kwa yako maghani, usikome sema.

Sema zitaje gharuri, duniya ni dema,

Sema na maghubari, duniya ni rima,

Sema duniya hatari, mwina wa nakama,

Sema sema kwa yakini, wasa ghaya sema.

Sema kwani hamwoni, walioachwa nyuma?

Sema pasi taraghani, uliyoyasema,

Sema wachuma tumboni, ja minyoo sema,

Sema sema mwafulani, u salama sema.

**Maswali**

a) Toa mifano miwili ya idhini ya kishairi katika shairi hili. (alama 2)

b) Tambua bahari zozote nne zinazopatikana katika shairi hili na utoe sababu.(alama 4)

c) Onyesha jinsi mshairi alivyofaulu kutumia mbinu ya kiusawe katika shairi. (alama 2)

d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

e) Tambua nafsinenewa. (alama 2)

f) Eleza sifai za kiarudhi katika ubeti wa pili. (alama 4)

g) Andika ubeti wa tano katika lugha nathari. (alama 4)

## SEHEMU YA E (Alama 20 )

### FASIHI SIMULIZI

5. 7. a) Vitendawili ni nini? (alama 2)

b) Eleza aina tatu ya vitendawili. (alama 6)

c) Eleza sifa tano za vitendawili. (alama 5)

d) Fafanuai majukumu saba ya vitendawili. (alama 7)